TAREHE YA AL-IMAM AL-HABIB AHMAD MASHHOOR BIN TAHA AL-HADDAD KWA UFUPI

Imeandikwa na: As-Sayyid Muhammad bin Mustafa Abunumay (mjukuu wa Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad)

** Jalada la mbele ni sura ya Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddaad iliyopigwa picha na Abdulalim Essa* Ayub

Utangulizi imeandikwa na **As-Sayyid Mustafa bin Alwy Abunumay**
Mwandishi wa kitabu ni **As-Sayyid Muhammad bin Mustafa bin Alwy Abunumay**

Kwa niaba ya **As-Sayyid Muhammad bin Mustafa Abunumay**, kitabu hichi imechapishwa na **Abdulalim Essa Ayub**

Rasimu na **Ahmad Abdulalim Essa**

Kitabu hiki kimechapishwa na **PAFAX Printers & Stationers**, **UK**

Shawwaal 1442 AH / June 2021 CE



Nyumba ya Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad

(Chumba ya wageni)

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad pamoja na mjukuu wake As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay anaingia Msikiti wa Sheikh Jundani kwa Swala ya Ijumaa

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Shukrani zote ni kwa Mwenyeenzi Mungu ﷻ. Kufaulu ni kutoka kwake ﷻ. Hakika amefaulu katika kuifanya kazi nzuri hii ya kukusanya na kuandika juu ya maisha ya Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad na kazi yake kubwa aliyoifanya katika kusambaza, kuusomesha na kuusimamia Uislamu hasa katika pande za Africa ya mashariki. Nina furaha na kukushukuruni mlonipa heshima hii ya kuandika utangulizi huu kwa kazi hii aloifanya mwanangu Muhammed Mustafa Alwi Abunumey.

Kazi hii inayoeleza maisha yake mwanachuoni Al-Imam Al-Habib Ahmad Mashhoor imeitwa fupi lakini katika ufupi wake imekusanya mengi na kwa usahihi juu ya tokea kuzaliwa kwake, maisha yake Hadhramout, safari zake Indonesia, kazi kubwa ya kuujenga na kuusomesha Uislamu katika Afrika ya Mashariki, hatimaye kurudi kwake na kuishi Jeddah, Saudi Arabia alikofariki dunia na kuzikwa Makka. Sina moja la kuongeza au la kukosowa katika kazi hii ilofanywa.

Utangulizi huu ni mfupi, lakini watosha kwa kuipa umuhimu na kuibarikiya kazi hii ya Al-Marhum mwanangu Muhammed juu ya babu yake. Nawaombea Mwenyeenzi Mungu awarehemu yeye na babu yake Al-Habib Ahmad Mashhoor Al-Haddad. Awajaalie kheri na wawe kwenye kila lilo jema huko waliko. Amin. Na sisi huku tusomao kazi hii ya maisha ya bwana huyu mtukufu tupate baraka na ilmu zake.

As-Sayyid Mustafa bin Alwy bin Ahmad Abunumay

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

SHUKRANI

Baada ya kumshukuru Allah ﷻ na kumtakiya rehma na amani Mtume wetu Sayyidina Muhammad ﷺ, nimebarikiwa sana kwa kupatiwa fursa kama hii ya kuweza kuchapisha hii tarekh ya Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad ambayo imetungwa na mjukuu wake As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay tarehe tatu (3) mwezi wa Dhul-Hijjah mwaka wa 1417 Hijria (21.04.1996).

Niliporegea Mombasa mwaka wa 1421 Hijria, As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay alinipatia kitabu hicho pamoja na baadhi ya picha za Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad ambazo kwamba nilizipiga mimi na kunielezea namna ya kupanga kitabu hicho.

Nimemjua As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay tangu udogoni mwake alipokua akilelewa na babu yake Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad. Aliendelea masomo yake mji wa Tarim kwa muda wa miaka nne (4) kisha akaregea Mombasa na kufungua Madrasa yake maaruf kwa jina ya "Madrasatul Faqih Al-Muqaddam". Alisomesha wanafunzi na kunufaisha wengi kabla ya kuondoka kwake duniani tarehe ishirini (20) mwezi wa Shawwal mwaka wa 1423 Hijria. Ijapokuwa aliondoka akiwa na umri mdogo alifanya kazi kubwa kwa Ummah na amewacha mengi yenye kutunufaisha.

Baada ya kumaliza kupanga hii tarehe, niliituma kwa babake, As-Sayyid Mustafa bin Alwy Abunumay, ili aandike utangulizi na ningependa kumshukuru as-Sayyid Mustafa shukrani ya dhati.

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliosaidia katika kuwezesha kitabu hiki kumalizika, kwa majina:

1. Sayyid Adnaan bin Ali bin Ahmad Mashhur Al-Haddad
2. Sayyid Mustafa bin Alwy Abunumay
3. Sayyid Muhammad bin Muhammad bin Mustafa Abunumay
4. Ustadh Jaafar As-Sadiq bin Muhammad bin Shareef Saeed Al-Beidh
5. Shaykh Sulaiman Salim
6. Shaykh Fadhil bin Abbas Al-Jahdhamy
7. Shaykh Omar bin Swaleh Eleyyan
8. Shareef Omar bin Mohammad bin Abraar An-Nadhiry
9. Sayyid Tahir bin Mohammad Abunumay
10. Sayyid Talib bin Athman bin Mohammad Jamalul-Layl
11. Dr. Yaakub AbdulHamid Sheikh
12. AbdulRahim bin Muhammad bin Ali Al-Maawy
13. Mohammad bin Saeed bin Mohammad Al-Jahdhamy
14. Anwar Osman
15. Ahmad Abdulalim Essa

بسم الله الرحمن الرحيم

Jina Lake

Ni Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha bin Ali bin Abdallah bin Taha bin Abdallah bin Taha bin Umar bin Alwy bin Mohammad Al-Haddad

Kuzaliwa Kwake na Malezi Yake

Al-Habib Ahmad Mashhoor alizaliwa katika mji wa Qaidun, Hadhramout, Southern Yemen mwaka 1325 Hijria – 1907 Miladia. Wakati huo babake alikua amesafiri kwenda Indonesia. Alikulia katika nyumba ya ilmu na malezi ya kidini. Kwani mamake ndie mwalimu wake wa mwanzo aliemsomesha Qur'ani na baadhi ya mafunzo ya kidini. Mamake ni Hababa Swafiyyah bint Twahir bin Omar Al-Haddad, alikua ni katika bibi ambae amehifadhi Qur'ani tukufu na mcha mngu mkubwa sana.

Al-Arif Billah Al-Habib Taha bin Ali Al-Haddaad
(Babake Al-Habib Ahmad Mash-hoor Al-Haddaad)

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddaad

Kusoma Kwake

Alipofika umri wa kufahamu mamake alimuingiza katika "Ribaat" (chuo cha dini) iliokua wakati huo hapo Qaidun. Alisoma kwa ammi zake Al-Habib Abdallah bin Twahir na Al-Habib Alwy bin Twahir Al-Haddad. Alisoma kwa mabwana hawa wawili ilmu ya Fiqhi (Islamic Law), Tafsiri, Hadith, Nahwu, Swarfa, Balagha, Usulul-Fiqh, Tasawuf na masomo mengine. Alikua ni katika wanafunzi wekevu na wenye bidii sana, mpaka masheikhe zake walimuekea darasa za ziada kumsomesha peke yake na kumtanguliza kuliko wanafunzi wenzake.

@Picture Courtesy by Sayyid Adnan al-Haddad

Al-Allamah Al-Arif Billah Al-Habib Abdallah bin Twahir Al-Haddaad

Al-Allamah Al-Muhaddith Al-Habib Alawi bin Twahir Al-Haddaad

Ribaat ya Qaidun – Al-Habib alisoma hapa



Al-Allamah Al-Muhaddith Al-Habib Alwy bin Twahir Al-Haddaad *(Mufti wa Johor, Southern Malaysia)*

Safari Yake ya Kwanza

Alipofika umri wa miaka kumi na nane (18) sheikhe wake Al-Habib Alwy bin Twahir Al-Haddad alimchukua kwenda nae indonesia, huko alisoma na kuchukua mafunzo na malezi ya kidini ya Ki-Islamu kwa wanazuoni wakubwa walikua huko wakati huo kama Al-Imam Al-Habib Mohammad bin Ahmad Al-Muhdhar, Al-Habib Abdallah bin Muhsin Al-Attaas, Al-Habib Alwy bin Mohammad Al-Haddaad na wengineo.

Baada ya miaka mitatu Al-Habib Ahmad Mashhoor alirudi Qaidun – hali amejaa maarifa na ilmu kubwa. Walimu na masheikhe wake walimkubali na wakamruhusu asomeshe katika Ribaat ya Qaidun.

Al-Habib Mohammad bin Ahmad Al-Muhdhar

Al-Habib Abdallah bin Muhsin Al-Attaas

Al-Habib Alwy bin Muhammad Al-Haddaad

Masheikhe Zake Wengine Katika Hadhramout

Hapo Qaidun hakutosheka aliingia mji baada ya mji katika Hadhramout kuzidisha ilmu yake:

Katika mji wa Quweira: alichukua kwa Al-Habib Mustafa bin Ahmad Al-Muhdhaar

Katika mji wa al-Qarain: alichukua kwa Al-Habib Omar bin Ahmad Al-Baar.

Katika mji wa Huraidha: Al-Habib Muhammad bin Salim Al-Attaas.

Katika Shibaam: Al-Habib Mustafa bin Abdallah bin Sumeit.

Katika Howta: Al-Habib Omar bin Abdallah Al-Habshy

Katika Seiyun: Al-Habib Ahmad bin AbdurRahman As-Saggaaf, Al-Habib Muhammad bin Ali Al-Habshy na Al-Habib Muhammad bin Haadi As-Saggaaf

Katika Tareem: Al-Habib Ali bin AbdurRahman Al-Mashhoor, Al-Habib Abdallah bin Omar Ash-Shatry na Al-Habib Alwy bin Abdallah bin Shihaab.

Katika Inaat: Al-Habib Hassan bin Isma‘il Al-Hamid.

Al-Habib Mustafa bin Ahmad
Al-Muhdhaar

Al-Habib Ahmad bin AbdurRahman
As-Saggaaf

Al-Habib Omar bin Abdallah
Al-Habshy

Al-Habib Muhammad bin Haadi
As-Saggaaf

Al-Habib Muhammad bin Ali
Al-Habshy

Al-Habib Alwy bin Abdallah
bin Shihaab

Baada ya hapo alikwenda pwani ya Hadhramout, Mukalla akachukua kwa Sheikhe wake mkubwa Al-Imam Ahmad bin Muhsin Al-Haddaar alipata kwa bwana huyo faida nyingi na ma-angalizi makubwa.

Al-Aarif Billah Al-Imaam Al-Habib Ahmad bin Muhsin Al-Haddaar

Safari Yake ya Kwanza Afrika Mashariki

Katika mwaka 1347 Hijria – 1926 Miladia, Al-Habib aliwasili Zanzibar kwa mara ya kwanza na akashukia kwa Sayyid Abdallah bin Haroon Baharoon na wakati Zanzibar ilikuwa imejaa wana zuoni wakubwa wakubwa kwa mfano Sheikh AbuBakar bin Abdallah Bakathir, Sheikh Mohsin bin Ali Al-Barwaany, Sayyid Abul-Hasan bin Ahmad Jamalillayl, Sheikh Burhanuddin bin Mohammad Al-Mukallah na wengineo wa madhehebu mbali mbali, wanazuoni hawo walimpenda na kumtukuza.

Baada kuiona ilimu yake – ilipatikana baina yake na Sheikh Qaswar – Sheikhe mkubwa wa Ki-Ibadhi majadiliano kuhusu utungaji wa mashairi ya kiarabu – bwana kama huyo alimuliza Al-Habib Ahmad Mashhoor baadhi ya maana ya undani ya mashairi ya Sheikh Ibnul-Faridh mshairi maarufu na Al-Habib Ahmad Mashhoor alimjibu kishairi jawabu ya kutosha kabisa. Hapo Sheikh Qaswar alishangaa na kuona ajabu – kwa jawabu kama hiyo kutoka kwa kijana wa miaka ishirini na mbili (22), ilihali yeye mwenyewe ni wa umri takriban miaka sabini (70). Hapo Sheikh Qaswar alimkubali kama Al-Habib Ahmad Mashhoor amekamilika katika lugha ya kiarabu na alla zake zote – hapo wanazuoni wa Zanzibar walimtambua Al-Habib Ahmad Mashhoor. Wakamuomba awaekee darasa ya tafsiri ya Qur'an katika mwezi wa Ramadhaani katika Msikiti wa Ijumaa Malindi – hapo ilionekana ilmu yake yakutafsiri na kueleza neno lake la Mwenye-Enzi Mngu: "**Iyyaaka na'budu wa iyyaaka nasta'in**" kwa muda wa siku kumi na tano (15). Baada ya muda wa miezi sita (6) Al-Habib Ahmad Mashhoor alirudi zake Hadhramout.

Nyumba ya As-Sayyid Abdallah bin Haroon Baharoon huko Zanzibar

As-Sayyid Abdallah bin Haroon Baharoon

Ash-Sheikh AbuBakar bin Abdallah Bakathir



Ash-Sheikh Mohsin bin Ali Al-Barwaany

As-Sayyid Abul-Hassan bin Ahmad Jamalil-Layl

Ash-Sheikh Burhaanuddin bin Mohammad Al-Mukallah (Sheikh Burhan Mkelle)

Safari Yake ya Pili Afrika Mashariki

Katika mwaka 1351 Hijria – 1930 Miladia alirudi kwa mara yake ya pili – aliingia Mombasa na kushukia kwa Sheikh Swaleh bin Salim Eleyyaan – mtaa wa Makadara – hapo Mombasa alisikia habari na swifa za Al-Habib Swaleh bin Alwy Jamalil-layl wa Lamu, alifunga safari akenda Lamu kwa meli "S/s Dumra". Alipofika Lamu Al-Habib Swaleh alimpokea kwa taadhima na hishima kubwa. Wakati wa Swala ya Adhuhuri. Al-Habib Swaleh mwenye umri wa miaka thamanini (80) wakati huo alimtanguliza kijana wa umri wa miaka ishirini na sita (26) kuswalisha, hii inaonesha utukufu wa ilmu na daraja alizokua nazo Al-Habib Ahmad Mashhoor kutangulizwa na bwana kama huyo.

Baada ya kukaa Lamu kwa muda mchache aliazimia kurudi Mombasa ili kuifunga safari ya kwenda Hija. Al-Habib Swaleh alimwabia "Kama ukenda Mombasa hutopata safari bora, wende Kismayo utapata safari". Hapo Al-Habib Ahmad Mashhoor alifuata ishara aliopewa na Al-Habib Swaleh. Hapo akaondoka kwa jahazi pamoja na Sayyid Ali Badawy na Sayyid Omar bin Alwy Al-Aideed kwenda Kismayo kwa njia za Bajunini – Kismayo akapata meli inayokwenda Jeddah.

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad alishukia nyumba hii ya Sheikh Swaleh bin Salim Eleyyaan mtaa wa Makadara, Mombasa

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad na Sheikh Swaleh bin Salim Eleyyaan

Kuishi Kwake Mombasa



Sheikh Abdallah bin Mohammad Al-Husny

Katika mwaka 1351 Hijria (1930 Miladia) baada ya kurudi Al-Haji alibakia Mombasa alikaa katika mtaa wa Mji wa Kale. Alianzisha biashara ndogo pamoja na kufundisha na kueneza dini. Alifungamana na mwana chuoni mkubwa Sheikh Abdallah Al-Husny na wakawa wanashirikiana pamoja katika kazi ya kueneza dini nje ya mji na vitongoji kama pande za Digo na Giriama. Katika mji wa Mombasa alikua na darasa wakati tafauti tafauti, kama asubuhi alianza nyumbani kwake, alasiri Msikiti Mwijabu, magharibi Msikiti Nuru, na Khutba ya Ijumaa na Swala Msikiti Khonzi. Hamu yake kubwa ilikuwa ni kueneza dini, ama biashara aliifanya kwa sababu ya kuhifadhi nasfi yake na dini yake kama walivyokua baadhi ya masahaba wa Mtume ﷺ na baadhi ya wanazuoni wakubwa waliotangulia kwa mfano wa Al-Imam Abu-Hanifa na Al-Imam Abdallah Ba'Alawy na wengineo.

Al-Habib na Sheikh Al-Amin bin Ali Al-Mazrui

Sheikh Al-Amin bin Ali Al-Mazrui

Al-Habib Ahmad Mashhoor alikua na mafungamano na mahaba makubwa baina yake na Mufti wa pwani Al-Sheikh Al-Amin bin Ali Al-Mazrui. Sheikh Al-Amin akimpa hishima na akimtukuza Al-Habib Ahmad Mashhoor na alikua akimsifu kwa kusema, "Al-Haddad alifika vilele vya nyanja zote za elimu na hekima". Alikuwa Sheikh Al-Amin akitoka kwake Kibokoni asubuhi kwenda Mji wa Kale – na walikua wakisomeshana. Al-Habib Ahmad Mashhoor alikua akisoma ilmu ya 'Miqati' na Sheikh Al-Amin alikua akisoma kutoka kwa Al-Habib ilmu ya 'Mantiq' (logic). Katika jumla ya mambo yenye kuonesha nguvu ya mafungamano baina ya mabwana hawa wawili nikua Sheikh Al-Amin aliusia akasema hastahiki mtu yoyote baada yake katika Umufti na kuchukua cheo cha uchifu Qadhi illa Al-Haddad.

Baada ya kufariki Sheikh Al-Amin alitaka Al-Habib Ahmad Mashhoor achukue mahali pake, yeye aliikataa kazi hiyo na kusema "Sisi kazi yetu ni Da'wah na kuongoza watu katika njia ya Mngu". Na katika mabwana alio fugamana nawo Al-Habib Ahmad Mashhoor na kuchukuwa kwao katika Afrika Mashariki ni Al-Imam Al-Habib Omar bin Ahmad bin Sumeit aliye kuwa Kadhi mkuu wa Zanzibar kutoka 1935 mpaka 1964. Al-Habib Omar alikuwa akimpenda sana Al-Habib Ahmad Mashhoor na kumuongoza katika kazi zake alizokuwa akizifanya katika Da'wah popote pale alipo. Alikua akimsifu na kuambiya watu kuwa Al-Haddad adiye Khalifa na shekhe wenu baada yangu. Al-Habib Omar alifariki katika kisiwa cha Ngazija (Comoro Islands), tarekhe 9th Safar 1396 Hijria (Tuesday 9th Febuary 1976)

Al-Imam Al-Habib Omar bin Ahmad bin Sumeit

Picha hii ilichukuliwa katika mwezi wa Muharram 1382 Hijria sawa na 1962 Miladia hapo Unguja (Zanzibar)

Al-Habib Omar bin Ahmad bin Sumayt, muongozi wa Kiislamu maarufu ndani ya Afrika mashariki na Hadhramout, alikuwa Mombasa (mwezi wa Mei 1965) kuelekea Hadhramout. Al-Habib Omar akafanya ziara fupi kisiwa cha Comoros sehemu alikozaliwa mwaka wa 1886. Sayyid Mohammad bin AbdulRahman Al-Sheikh Abubakar bin Salim, Kadhi mkuu wa Comoros, alisafiri kwenda Mombasa kwa ndege ya kukodi khususan kuandamana na Al-Habib Omar. Al-Habib Omar alikuwa Kadhi mkuu wa Zanzibar hadi alipostaafu na hapo kuazimia kurudi Hadhramout milele. Waliochukuliwa picha uwanja wa ndege wa potrizi Mombasa katika kumuaga ni Sayyid Mohammed Abdulrahman Al-Sheikh Abubakar bin Salim (Kadhi mkuu wa kisiwa cha Comoros), Maalim Said Ahmad Al-Kumry wa Mombasa, Shariff AbdulRahman Khitamy, Al-Habib Omar bin Ahmad bin Sumayt, Bwana Abbas wa E.A. Airways, Sayyid Mohammad bin Alwy Abunumay, Sayyid Mustafa bin Alwy Abunumay, Sheikh Swaleh Bin Salim Eleyyan wa Mombasa na Sayyid Sheikh bin Ahmad Al-Aydarus (mpwa wa Al-Habib Omar Bin Sumayt).

Picha imehifadhiwa na Sayyid Mohammad Mustafa Abunumay

As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay kaniambia niweke picha hii kwenye kitabu kwa sababu babake anaonekana

Al-Habib Ahmad Mashhoor Kwenda Uganda

Al-Habib Shareef Sa'id bin Abdallah Al-Beidh

Katika mwaka 1375 Hijria (1955 Miladia) Al-Habib Ahmad Mashhoor alikwenda Uganda kwa ajili ya Da'wah, na aliishi Kampala. Alikua Imamu na Khatibu wa Msikiti wa Nakasero, alishirikiana na watangazaji wa dini kama Al-Habib Shareef Sa'id al-Beidh walifanya jihadi kubwa ya kusilimisha watu, mpaka ikafika idadi kubwa ya watu kusilimu. Huko Uganda alitunga kitabu chake alichokiita "Miftahul Jannah" (Ufunguo wa Peponi) ambacho ameeleza maana ya "**Laa ilaaha illaal-Laah**" utukufu wake na umuhimu wake katika dini. Kitabu hichi sasa kimeenea ulimwengu mzima, sababu kimefasiriwa kwa Kiengereza, Kifaransa, Kijarumani, Ki-Urdu na Kiswahili.

Al-Habib Ahmad Mashhoor Kurudi Kenya

Baada ya kuondoka Uganda alirudi Kenya na kuishi Mombasa. Aligawanya muda wake kuka Suudia miezi sita (6) na hapa Kenya miezi sita (6) juu ya yote hayo, Al-Habib Ahmad Mashhoor hakuwacha kupigania dini na kuongoza watu katika njia ya Mwenyeenzi Mngu – alikua kila mahali afikapo akiweka madarasa ya ilmu, na akenda huku na kule katika miji na vitongoji kuangalia hali za Waislamu.

Kazi Zake za Kheri Alizofanya

Ilikua ni kujenga Misikiti pande za Digo ambayo ni hii

1. Masjid Bug-Shan - Likoni
2. Masjid Iddi Ndoro (Shika Adabu) - Likoni
3. Masjid Mwana Nyamala (Ramisi) - Kwale County
4. Masjid Nuru (Pungu) - Kwale County
5. Masjid Ngombeni - Kwale County

Masjid Bug-Shan

Masjid Iddi Ndoro

Masjid Mwana Nyamala

Na pia kuujenga upya mara ya pili Masjid Swalihina (Kisauni), Msikiti wa Gede pamoja na Madrasa, na chuo cha dini kiitwacho Al-Ghanna-ul-Islamiyyah – Mambrui.

Hii nido Masjid Swalihina, Kisauni - Mombasa

Nje ya mtazamo wa chumba cha kupumzika cha Al-Habib huko Madrasa Al-Ghanna ul-Islamiyyah - Mambrui

Nje ya mtazamo wa chumba cha kupumzika cha Al-Habib huko Madrasa Al-Ghanna ul-Islamiyyah - Mambrui

Hii ndio Masjid Al-Husna, Gede - Kenya

Hii ndio Madrasa Al-Husna, Gede - Kenya

Kazi hizo alizifanya pamoja na watu wa kheri waliojitolea kwa nafsi zao na mali yao kwa ajili ya Mwenye-Enzi Mngu. Al-Habib Ahmad Mashhoor hakuacha kusimamia majenzi kama hayo hadi safari yake ya mwisho. Katika mwezi wa Ramadhaani alikua na darasa katika Msikiti wa Khonzi – na miaka sita (6) yake ya mwisho alihamisha darasa yake kama hiyo nakupeleka Msikiti Sheikh Jundan. Na pia kila siku ya Ijumaa baada Swalatil-Jumaa alikua baada ya swala akiwaidhi katika Msikiti huo huo. Swala ya Taraawehe akiswalisha katika Msikiti wa Memon (Birikau), na akitoa darasa baada ya swala kwa muda wa miaka arubaini (40).



Hii ndio Masjid Khonzi (1980s)

Hii ndio Masjid Sheikh Jundani (1980s)

Darasa baadal Asri mwezi wa Ramadhaan - Msikiti Sheikh Jundani
1982-83

Darasa baadal Asri mwezi wa Ramadhaan - Msikiti Sheikh Jundani
1982-83

Umbo Lake na Tabia Yake

Al-Habib Ahmad Mashhoor alikua na kimo cha wastani, mweupe mwenye mwili wenye afya njema, usowake ukingara kwa nuru ya ilmu na taqwa, alikua na sauti nzuri yenye kuvutia, tabia yake alikua mpole, mnyenyekevu, mwenye bashasha, na nyumba yake ilikua milango wazi kwa yoyote kuingia. Mwenye kuhisi na kuhimili mambo ya Uislamu. Alikua mwingi wa kusoma Qur'an na kusoma vyuo vya ilmu – mpaka ikafika hadi ya kusoma kurasa mia (100) katika usiku mmoja. Na akipenda sana kurudi katika tafsiri za Qur'an na maneno ya wanazuoni, alikua hakubali aayah impite bila ya kufahamu maana yake nje na ndani. Ameishi umri wake wote katika kusoma na kusomesha alikua mtungaji wa mshairi mkubwa sana. Amewahi kutunga qasida tafauti tafauti katika mnasaba tafauti nazo ziko katika kuchapishwa, na ametunga khutba za Ijumaa, pamoja na nadhmi ya "Safinatul Najah", tarehe ya kuanza ilmu ya Hadithi na vitabu vyengine na kadhalika.

Al-Habib Ahmad Mashhoor Kuhamia Jeddah

Baada ya kuingia umri wa uzee katika mwaka 1412 Hijria (1992 Miladia) alihamia Jeddah, hakuwacha kuikumbuka Afrika – haswa Kenya na watu wake.

Ilipofika siku ya jumatano, tarehe 14th Rajab mwaka 1416 Hijria (6th December 1995) katika wakati wa Al-Asri aliaga dunia – baada ya kuishi umri wa miaka tisini na moja (91).

Aliswaliwa baada ya Swalatil Dhuhri katika Haram ya Makkah na kuzikwa Makaburi ya Al-Ma'alaa, alipozikwa bibi mkubwa wa Waislamu Sayyidatna Khadija رضي الله عنها mke wa Mtume Muhammad ﷺ.

Mazishi yake yalikua makubwa sana ambayo Makkah haijashuhudia mazishi kama hayo, sauti ya Tahlil ilikua kubwa na yenye kitisho wakati wakupelekwa kwenda kuzikwa, watu wa Makkah walishutuka wakawa wanauliza ni nani huyo alofariki. Mwana chuoni mkubwa wa Makkah Sayyid Mohammad bin Alwy Al-Maliki alisema siajabu Al-Habib Ahmad Mashhoor kuzikwa kwa Tahlili sababu yeye alizaliwa, na kusomeshwa, na yeye kusomesha "**Laa ilaaha illaal-Laah**" na sasa ashindikizwa kwa hiyo hiyo "**Laa ilaaha illaal-Laah**" mpaka kaburini.
Dunia ilingia huzuni kubwa kuondokewa na bwana kama huyo, ambae alikua kiongozi mkubwa wa dini na ajulikanae dunia nzima. Amewacha wake wawili na watoto watano wa kiume wa wakike saba pamoja na wajukuu na vitukuu wanaowkurubia mia moja (100). Mngu amrehemu Al-Habib Ahmad Mashhoor, ajalie kaburi yake kuwa bustani katika bustani za peponi – na asitukoseshe baraka zake na ilmu yake na mwendo wake - Aameen.

Imekusanywa na kuandikwa na mjukuu wake As-Sayyid Muhammad Mustafa Alwy Abunumay imesahihishwa kilugha na kurejewa na As-Sayyid Hassan Alwy Al-Ahdaly (Jombi)
(3rd Dhul-Hijjah 1417 Hijria – 21st April 1996 Miladia)

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akiwa na mjukuu wake, As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay. Hapo wanatoka Msikiti Sheikh Jundani baada ya Swala ya Ijumaa

As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay akimbusu mkono ya babu yake Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad - *1985*

Hapa nyumbani kwa Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad, baada ya Swala ya ‘Idd ya mfungo-mosi (‘Idd al-Fitri)

Hapa nyumbani kwa Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad, baada ya Swala ya ‘Idd ya mfungo-mosi (‘Idd al-Fitri)

Kisomo cha Ihda 'Ashariyyah nyumbani kwa As-Sayyid Swaleh Abdallah Taib - Old Town. Shareef Twaha Al-Haddad, Mwenye Karama, Shareef Khitamy, Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad, Sayyid Ahmad Ahdal na Ustadh Mohammad Al-Beidh - *1987*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad na Shareef AbdulQaadir bin Isma'il Al-Hamid na Shareef Twaha bin Ali Al-Haddad

Nyumbani kwa Hababa Sharifa (Masheri). Hawli ya Al-Imaam Al-Habib Alwy bin Abdallah bin Shihaab, tarehe 12 mwezi wa Ramadhaan baada ya Swala ya Taraaweh - *1985*

Nyumbani kwa Shareef Twaha, Nairobi West, alipowasili Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad baada ya kutoka Hijja.
1989

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad na Chief Kadhi wa Kenya, Sheikh Nassor Nahdy, kwenye sherehe ya ufunguzi wa Masjid Al-Falah, Likoni, katika mwezi mtukufu wa Ramadhaan - *1986*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akiwa Malindi. Upande wa kushoto Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad, Shareef AbdulQaadir Al-Hamid na Sheikh Islam Magram. Upande ya kulia Sheikh Mohammad bin Ali Al-Amoody na Shareef Ahmad bin Muhammad Al-Beity - *1972*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad kwenye sherehe ya kuweka jiwe la msingi la Madrasa Dar-ul-Uloom, Masjid Hidaya - *1987*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad kwenye sherehe ya kuweka jiwe la msingi la Madrasa Dar-ul-Uloom, Masjid Hidaya - *1987*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad na Sayyid Ali Badawy, wakiwa kwenye hafla ya kusoma Burda nyumbani kwa Sheikh Mahmood Mohammad Ali Al-Jahdhamy na ndugu yake Sheikh Khalid Mohammad Ali Al-Jahdhamy - *1984*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad na Sayyid Ali Badawy, wakiwa kwenye hafla ya kusoma Burda nyumbani kwa Sheikh Mahmood Mohammad Ali Al-Jahdhamy na ndugu yake Sheikh Khalid Mohammad Ali Al-Jahdhamy - *1984*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akiwa pamoja na Sheikh Sa'id Al-Jahdhamy na Sheikh Salim Al-Jahdhamy katika Msikiti wa Sheikh Jundani, katika siku kumi za mwisho za mwezi mtukufu wa Ramadhaan - *1985*

Darasa baada ya swala ya alasiri Msikiti wa Sheikh Jundani upande wa kulia ni Sheikh Swaleh Shigog, Shareef AbdulQaadir na upande wa kushoto ni Shareef Mwenye Karama na Sheikh Adam Sulaiman Mirjangi. - *1982-83*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha al-Haddad akiingia nyumbani kwa Sheikh Mohammad bin Ahmad Al-Jahdhamy wakati wa usiku ya Nisfu-Shabaan - *1985*

Wakati ya Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad kutembelea Masjid Sheikh Iddi Ndoro, Shika Adabu - Likoni, Sheikh Fadhil Abbas Al-Jahdhamy anamsaidia Al-Habib - *1982 - 83*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akitembelea Masjid Sheikh Iddi Ndoro, Shika Adabu - Likoni - *1982-83*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad alipowasili kwenye jumba la "Malindi Complex" kwa sherehe ya ufunguzi wa Msikiti Al-Ridha, Malindi, Kenya. - *1992*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad alipowasili kwenye jumba la "Malindi Complex" kwa sherehe ya ufunguzi wa Msikiti Ar-Ridha, Malindi, Kenya - *1992*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akiwa nyumbani kwa Shareef Twaha, Port-Reitz mwezi wa Ramadhaan baada ya Taraaweeh - *1983-84*

Al-Habib Ahmad Mashoor bin Taha Al-Haddad akiwa nyumbani kwa Shareef Twaha, Port-Reitz. Kutoka kulia Sayyid Jaafar, Sayyid Husayn, Shareef Taha, Al-Habib Ahmad Mashhoor Al-Haddad, Sayyid Zayn, Sayyid Ahmad, Sayyid Muhsin, Sayyid Mohammad Mustafa Abunumay

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akiwa kwa Shareef Twaha, Port-Reitz usiku wa 27th Ramadhaan 1986 baada ya swala ya Taraaweeh

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akiwa nyumbani kwa Shareef Twaha, Port-Reitz usiku wa 27th Ramadhaan 1413 Hijria sawa na 1st April 1992

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad kwa futari ya Ramadhaan baadal maghrib. Kutoka kulia: Sheikh Swaleh Shigog, Al-Habib Ahmad Mashhoor, Sheikh Swaleh Eleyyan, Mwidani (Mayor wa Mombasa), Sheikh Nahdy.

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akiwa Mckinnon Road baada ya kutoka Hijja - *1989*

Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad akiwa Mckinnon Road baada ya kutoka Hijja - *1989*

As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay pamoja na wanafunzi wake wa 'Madrasatul Faqih al-Muqaddam'.
Kutoka kushoto: Sayyid Dr. Adnan Muhdhir Al-Ahdaly, Dr. Yaakub AbdulHamid, Sayyid Nassir Ghalib, Shk Mohammad Awadh, Sayyid Mohammad Mustafa Abunumay, Shareef Abdallah Al-Wareeth, Abdillah Noor Mohammad, AbdulRahim Al-Maawy na Mohammad Mahmud.
Walioketi ni: Farooq Essa, Hamza AbdulRahman na Ali Mahmud.
2001

As-Sayyid Hasan bin Alwy Al-Ahdal (Jombi) pamoja na As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay
2001

وَلَقَيْنَا سِرَّ أَسْـــــــرَارِه وَاقْتَبَسْنَا نُوْرَ أَنْـــــــوَارِه
وَاجْتَمَعْنَا فِي رِحَابِ الـطُّوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

طَيِّبُ الْأَفْعَالِ وَالْأَخْـــلَاق عِلْمُهُ قَدْعَمَّتِ الْآفَـــــاق
فِي جَمِيْع بُلْدَانِنَا مَنْـــــشُوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

سِرُّهُ يَسْـــــــرِي لِأَوْلَادِه وَلِأَسْبَاطِـه وَأَحْفَـــــادِه
وَمُحِبِّيهِ الَّذِى فِي الـــدُّوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

حُبُّهُ قَدْ حَلَّ فِي قَلْبِـــــي إِنَّ هَـذَا الْفَضْـــــلَ مِنْ رَبِّي
سِرُّهُ فِي مُهْجَتِي مَسْـــطُوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

يَا حَبِيْبِي قُمْ بِنَا بَـــــادِرْ كَيْ نَظْفِرْ دُنْيَـــــا وَالْآخِرْ
هَيَّـا هَيَّـا أَحْمَدَ الْمَشْـــهُوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

رَبِّ فَانْفَعَنَا بِبَرَكَاتِـــــــه وَاعْطِنَا مِنْ سِرِّ نَفَحَاتِـــــه
وَاعْطِنَا مِنْ حَظِّهِ الْمَوْفُـــوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

ثُمَّ صَلُّوا عَلَى الْمَحْـــبُوْب مَنْ بِهِ يَحْصُلُ الْمَطْـــلُوْب
كُلُّ عَاصِي ذَنْبُهُ مَغْـــفُوْر بِابْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

وَعَلَى آلِهِ وَأَصْحَابِـــــــه ثُمَّ أَتْبَاعِه وَأَحْـــزَابِـــــه
عَـدَّمَا زَائِرْ أَتَى بَايَـــــزُوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

Qasida hii imetungwa na As-Sayyid Muhammad Mustafa Abunumay kumtukuza babu yake, Al-Imam Al-Habib Ahmad Mashhoor bin Taha Al-Haddad رضى الله عنه

بسم الله الرحمن الرحيم

الله الله الله الله الله الله الله الله

نَتَوَسَّلْ بِالنَّبِيِّ النُّـــــوْر وَابْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْهُـــــوْر

يَا كَرِيْمَ الْجُوْدِ يَا مَنَّـــــان يَا جَزِيْلَ الْفَضْلِ وَالْإِحْسَـان
أَمْلِ قَلْبِي بِالصَّفَا وَالنُّـــوْر بِابْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

رَبِّ سَهِّلْ كُلَّمَا رُمْنَـــــــا وَاعْطِنَا الْخَيْرَاتِ وَالْحُسْنَـــا
رَبِّ وَاجْعَلْ وَقْتَنَا مَسْـــرُوْر بِابْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

قَدْ تَوَسَّلْنَا بِخَيْرِ النَّـــــاس وَابْنِ عَلَوِي الْقُطْبِ وَالْعَطَّاس
وَالْوَلِيِّ ذُخْرَنَا الْمَشْـــــهُوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

سَيِّدِي أَحْمَدْ عَظِيْمِ الشَّـان مَعْدِنِ الْأَسْرَارِ وَالْعِرْفَـــان
فَيْضُهُ مَا بَيْنَنَا مَـــــدْرُوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

كَانَ فِيْنَا بَدْرُنَا السَّـاطِـــعْ وَكَسَانَا عِلْمَهُ النَّـــافِـــعْ
وَبِعَيْنِ الْمُصْطَفَى مَنْـــظُوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر

كَمْ رَوَيْنَا عَنْهُ مِنْ عُـــلُوْم وَشَرِبْنَا كَاسَهُ الْمَخْـــتُوْم
أَمْرُنَا طُوْلَ الْمَدَى مَيْسُوْر إِبْنِ طٰهٰ أَحْمَدَ الْمَشْـــــهُوْر